KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA

# Hotuba ya Kufunga Mkutano wa Wachungaji 2016

Imetolewa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo

## UTANGULIZI

Namshukuru sana Mungu kwa kutuwezesha kuwa pamoja kwa muda wote wa Mkutano wa Wachungaji wote wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Mkutano umekuwa wa baraka sana. Nawashukuru wote waliofika kwani tumebarikiwa sana na kila mtu kwa namna moja au nyingine ameuona utukufu wake Mungu.

Huzuni yangu ni kwa wale ambao hawakufika, tuzidi kuwaombea wote ili wakati mwingine waweze kuona umuhimu wa mkutano wetu huu katika kujenga umoja wetu. Wapo pia mababa Askofu ambao hawakufika na Wachungaji wao wamefika wachache sana.

Tumetafakari na kukumbushana kuhusu ‘umoja na ushirikiano kama Kanisa la Yesu Kristo hapa nchini. Mkutano umefanyika wakati tukielekea kukumbuka ‘Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa’ hivyo tumetafakari kwamba ‘Matengenezo ya Kanisa’ yana maana gani kwetu sisi Kanisa la leo.

## HOFU NA MASAHAKA

Moja ya mbinu anazotumia yule mwovu ni kuwajaza watu wa Mungu hofu na mashaka kuhusu mambo ambayo Mungu amekwishawapa; ili kulivuruga Kanisa la Mungu. Kuanzia katika Kitabu cha Mwanzo Mungu ameahidi kutupa mambo mema. Wasiwasi juu ya hilo hufanya mtu ajihoji kama hilo analotupa Mungu ni jema au kuna jema jingine?

Na ndiyo tuliyoona katika mafundisho yetu kwamba yule mwovu anaweza kutusahaulisha uzuri uliopo katika mafundisho yetu ya Kilutheri kuhusu Matengenezo, hivyo akatudangaya na vitu vyenye matunda au matokeo ya muda mfupi ambavyo si vitu vinavyotupa uzima wa milele, kama alivyosema Askofu Dkt. Abednego Keshomshahara (alipofundisha Neno Kuu la Mkutano wa Wachungaji 2016).

## MATENGENEZO

Tunaelekea kuadhimisha Kumbukumbu ya Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa huku tukiona kila dalili ya hali iliyokuwepo kabla ya ‘Matengenezo’. Hali ya watu kuwa na wasiwasi badala ya kuwa na uhakika; watu kujazwa hofu zisizo na msingi na watu kuingizwa katika mafundisho yasiyoendana na ukweli wa Neno la Mungu.

Nyakati hizi zinafanana ilivyokuwa kabla ya matengenezo. Watu wana mahangaiko mengi kama ilivyokuwa wakati wa kina Johann Tetzel (1465–11 August 1519) waliobuni mbinu mbalimbali za kuwadanganya watu ili waweze kujitajirisha.

Tunaona pia sasa hivi kuna bidhaa nyingi zinauzwa kwa jina la Yesu. Na bidhaa hizi kwa masikitiko makubwa, ni pamoja na wokovu tunaopewa kwa neema ya Mungu tu.

Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere aliwahi kutoa mfano wa watu wapumbavu waliokuwa wanauza almasi; akatokea mtu mmoja akatafuta namna ya kuwadangaya. Akaenda kuchonga vipande vya chupa za rangi mbalimbali na kuwaambia kwamba walizonazo si almasi ila alizonazo yeye ndio almasi za kweli.

Na wale watu kwa kutotambua uzuri wa walichokuwanacho, wakadharau almasi eti kwa kuwa tu mtu huyo alikuwa na makeke. Wakasema, ‘si ajabu hizi tulizonayo siyo almasi;’ wakapokea vipande vya chupa na kubadilishana na zile almasi za kweli. Inawezekana ndio kitu tunachofanyika sasa hivi.

Napenda niwaambie si kila king’aacho ni dhahabu. Siyo kila mtindo unaokuja sasa unafaa kuigwa. Ningependa baada ya mkutano huu turejezwe kama tulivyoelekezwa katika mafundisho ya msingi ya Ulutheri wetu. Kwanza tuone wema wake, tuone uzuri wake na ubaya wake kabla ya kuwapokea wanaokuja na vitu, mitindo au mbwembwe za kila aina.

## WAJIBU WETU

Tunapofunga mkutano huu kama mtumishi wa Mungu, uwe Askofu au Mchungaji, jiulize: 'Nina nafasi gani na nimeweza kufanya nini ili kuimarisha umoja wetu?' Kila mmoja ana nafasi yake. Baada ya mafundisho yaliyotolewa hapa, kila mmoja ajiulize swali hili: 'Ni kwa namna gani, kwa kujua au kutokujua nimekuwa kikwazo au nimekuwa sababu ya kuharibu umoja wa Kanisa letu?'

Iwe ni wale tulio na nafasi ya Askofu; Wajumbe wa Halmashauri Kuu au iwe ni sisi Wachungaji jiulize: 'Kuna mahali ambapo nimekuwa sababu ya kuharibu umoja wetu, nimekuwa kikwazo kinyume kabisa na ndoto na maono waliyokuwa nayo wazee wetu wale walioanzisha umoja wa makanisa saba na kuunda KKKT?

Na kwa yale mambo ambayo Roho Mtakatifu ameniangazia katika Mkutano huu wa Wachungaji, labda ni kwa tofauti ya mtazamo ambayo ninaona kwamba nahitaji kubadilika, je niko tayari kubadilika?' Naomba Bwana Yesu na Roho Mtakatifu akatuwezeshe kwenda kuyatenda yale mambo ambayo yatajenga umoja wa Kanisa letu.

## TUKATIMIZE AHIDI

Tumeshiriki pamoja 'Meza ya Chakula cha Bwana' na tumepokea msamaha wa dhambi zetu pale tulipokosea; hivyo sasa twende na nguvu mpya tukatende hayo tuliyoahidi kutimiza kwa pamoja katika kuimarisha umoja wetu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania. Naomba tunapoondoka tukawe tayari kutenda na tukaone mabadiliko. Namsihi sana Mungu hata na kwa wale wenzetu ambao hawajahudhuria ninyi muwapelekee salamu zetu na zisiwe za maneno bali za matendo kwa mabadiliko katika utendaji wetu. (Makofi).

## MKUTANO WA FMKD

Mwaka 2017 kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) utakaofanyika Windhoek, Namibia. Mada kuu: 'Nimekombolewa kwa neema ya Mungu' (Liberated by God's grace). Kwa kuwa tunakombolewa kwa neema, hivyo mkutano una mada ndogo ndogo tatu: 'Wokovu sio wa kuuzwa' (salvation is not for sale); 'Uumbaji siyo wa kuuzwa' (creation is not for sale) na 'Wanadamu sio wa kuuzwa' (human beings are not for sale).

Tunapaswa kujikumbusha mara kwa mara kuwa tusifanye wala kuvigeuza vitu hivi hata siku moja kuwa biashara. Kila mmoja ana haki ya kufika mbele za Mungu kupokea neema, ambayo siyo ya kuuzwa (grace is not for sale).

## WOKOVU SIYO BIASHARA

Katika yale yote tuliyojifunza katika mkutano huu, ndugu zangu, naona lililo hatari kubwa sana ni hili la watu wakishajazwa hofu, wokovu nao unageuzwa kuwa biashara. Na hatari hii iko hata miongoni mwa baadhi ya watumishi wa Kilutheri kwa kuona kwamba wakati mwingine imeleta mapato makubwa kwa watumishi, basi na sisi tunataka kuiga hivyo.

Napenda kuwaambia utumishi wetu si kwa ajili ya kufanya biashara. Mungu ana namna nyingi za kututunza tukifanya kazi kwa uaminifu. Siyo kila mtindo tutaiga hata kama ni wa kupotosha eti kwa sababu unaleta watu wengi na kwa sababu unaleta mapato mengi. Tuwe waangalifu kwa hilo.

## MIGOGORO YA ARDHI

Tumesikia siku hizi kuna migogoro mingi ya ardhi. Tunasikia jinsi ardhi inavyopokwa na misitu inaangamizwa, eti kwa kuwa watu wanataka tu kufanya biashara. Tunasema Mungu ametupa uumbaji au dunia tuliyonayo ili tuweze kutenda haki; ili tuweze kuishi na kila mmoja ana haki ya kufurahia uumbaji wa Mungu na raslimali tulizopewa.

## BIASHARA YA BINADAMU

Tulifikiri kwamba biashara ya utumwa imekwisha duniani. Lakini kuna namna nyingine mpya ya utumwa au biashara ya binadamu. Hivi karibuni mmesikia kule Mkoa wa Mara kuna mwanamke aliyekamatwa na polisi akifanya biashara ya binadamu. Alikuwa anakusanya watoto na kutafuta soko; na bidhaa yake ni watoto wa kike. Alipohojiwa alisema mtoto mmoja alikuwa anamuuza kati ya Sh. 150,000/- hadi shilingi laki mbili.

Ninyi wenyewe mmesikia kwamba kuna biashara kubwa sana ya wanawake inafanyika duniani. Tuwe waangalifu na kukemea jambo hilo. Kuna roho ya biashara na roho ya kutafuta faida binafsi ambayo imetuingilia. Tukumbuke, tumekombolewa kwa neema.

## KUTUNZA KONDOO

Katika mkutano huu tumekumbushwa kuhusu wajibu wetu. Kwa kifupi mimi ningesema tumekumbushwa kwamba tunao wajibu na kwa kufundishwa na huyu aliye Bwana wa Kanisa. Ni ndani ya Yesu tu, na kwa kujiweka kweli chini yake, kwa unyenyekevu wote ndipo tutakapoweza kulilisha kundi lake; na kulitunza kama anavyotaka Yeye. Na hakuna njia nyingine ya kujifunza kwa Yesu zaidi ya kulishika sana Neno lake na kulitii; ndipo tutaweza kuwatunza watu wa marika yote kiroho kama anavyotaka Yeye.

## TUTUMIE TEHAMA

Tunaishi nyakati hizi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kama Kanisa na kama watumishi wa Mungu lazima tujiulize na kubuni mbinu za kutumia TEHAMA kwa manufaa na utukufu wa Mungu. Usikae mbali nayo kwa sababu wengine wanatumia kwa kutimiza malengo yao. Kwa hiyo umefika wakati ambapo tufikirie zaidi kuhusu mawasiliano.

## KUTOJIAMINI

La mwisho ninalotaka kusema ndugu zangu, tujiamini. Tujiamini kwa kuwa Bwana aliyetuita na ambaye tunamtegemea ni huyu Yesu Kristo aliyesema, amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Ninachoona miongoni mwa watumishi wengi wa Kilutheri ni hali ya kutojiamini. Wanajiuliza nimeitwa kweli? Au kwamba mimi ni mtumishi niliyepewa mamlaka yote na madaraka mbinguni na duniani?

Tumejidharau wenyewe tumejifanya wadogo sana ndio maana hata katika Ibada ya kawaida Mchungaji asiyejiamini anaweza kuachia madhabahu au mimbara ikachezewa na mtu ye yote.

Ukitaka kuona jinsi mchungaji asivyojiamini, utasikia wakati wa Ibada akisema lolote kwa Washarika atasema: ‘Naomba tufungue ukurasa fulani’; ‘naomba msimame’ au ‘naomba tuombe’. Wewe una mamlaka ndio maana tulikuwekea mikono. Badala yake waambie Washarika: ‘Kwa mamlaka niliyopewa na Yesu sasa msimame, sasa kaeni, sikilizeni Neno, au tuombe,’ (Makofi).

Hii kuomba omba inanipa picha kwamba tumejifanya wenyewe kuwa wadogo. Lakini hapa (katika mkutano huu) pia tumekumbushwa tusisababishe kudharauliwa kwa kujichanganya mno. Tusiwe wavivu mno na tusiwe wabinafsi mno. Hayo ndiyo mambo yanayomfanya Mchungaji, ambaye ni mtumishi wa Mungu, adharauliwe.

## KUHUISHWA UPYA

Basi ndugu zangu kwa kuwa katika faragha hii tumehuishwa upya na Roho Mtakatifu amezungumza nasi kipekee kwa njia mbalimbali; nasema kama mwana KKKT kwamba, mkutano huu umetusaidia kufanya upya agano la uaminifu katika utumishi wetu kwenye kujenga Umoja wa Kanisa letu.

Tumeshiriki pamoja Meza ya Chakula cha Bwana na tumepokea msamaha wa dhambi zetu pale tulipokosea. Ningeomba twendeni sasa tukiwa na nguvu mpya ya kutenda hayo tuliyoahidi kuyatimiza kwa pamoja katika kuimarisha na kuudumisha Umoja wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Nawaomba tutakapoondoka tukawe tayari kutenda na tukaone mabadiliko, namsihi sana Mungu juu ya hilo.

Kwa wale wenzetu ambao hawakufika, ninyi muwapelekee salamu zetu na zisiwe za maneno matupu; bali za matendo kwa kubadilika katika utendaji wetu. (Makofi).

Tuombeane sisi kwa sisi ili tuimarike katika huduma zetu.

**Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Fredrick Shoo** alitoa hii **Hotuba ya Kufunga Mkutano wa Wachungaji wa KKKT** uliofanyika Chuo Kikuu cha Dodoma **(UDOM),** 24 - 29 Septemba, 2016.